

MAELEKEZO NAMNA YA KUJAZA FOMU YA KUTEMBELEA KAYA

Jina la Fomu	Kutembelea kaya.
Utambulisho wa fomu	Fomu namba 3.
Madhumuni ya fomu	Ushauri nasaha juu ya lishe na matendo mengine wakati wa kutembelea kaya.
Mahali fomu itakapotumika	Kaya.
Mtekelezaji/Mtumiaji wa fomu hii	Mhudumu wa afya ya jamii ngazi ya kijiji.
Chanzo cha takwimu	Kaya.
Utaratibu wa kukusanya	Kila mwezi.
Namna ya usimamizi na uwasilishaji	Baada ya fomu hii kujazwa na kuihakiki, nakala moja ibaki kwa mhudumu wa afya ngazi ya kijiji, na nakala nyingine ipelekwe kwa msimamizi wa wahudumu wa afya ngazi ya kijiji.
Hatua za ujazaji fomu	Kumbuka: tumia herufi kubwa kwa ujazaji wa fomu hii.
	Fomu hii iorodheshe kaya zote zitakazotembelewa na kushauriwa juu ya lishe na matendo mengine, na hizo kaya zote ziwe zinazopatikana katika kitongoji kimoja. Kumbuka kutokuchanganya taarifa za kaya toka kitongoji kingine katika karatasi moja, endapo itatokea basi, anza karatasi mpya ajili ya kitongoji kingine.
	Kila mstari unawakilisha maelezo ya kaya moja iliyotembelea katika kitongoji.
	1. Hakikisha unajaza kwa usahihi maelezo yaliyoko juu ya fomu hii ikiwamo mwezi/mwaka wa ripoti, mkoa, wilaya, kata, kijiji/mtaa, kitongoji, jina na namba ya simu ya mhudumu wa afya ya jamii ngazi ya kijiji aliyetembelea kaya hizi.
	2. Andika tarehe ya kutembelea kaya kwa kufuata utaratibu huu: tarehe/mwezi/mwaka (xx/xx/xxxx).
	3. (Safu ya 1, 2, 3 na ya 4): andika idadi inayoonyesha jinsi ya kila mtoto kuanzia mwezi 0 hadi miezi 59 anayeishi katika kaya. Andika namba ndani ya kisanduku kinachoonyesha umri wa watoto.
	4. Safu ya (5): andika idadi inayoonyesha jinsi ya watoto wanaoishi kwenye kaya kuanzia umri wa miaka 5 hadi miaka 9.
	5. Safu ya (6): andika idadi ya wasichana wanaoishi kwenye kaya kuanzia umri wa miaka 10 hadi miaka 19.
	6. Safu ya (7): andika idadi ya akina mama wawawazito wanaoishi kwenye kaya.
	7. Safu ya (8): andika idadi ya wanawake wasio wawawazito wanaoishi katika kaya.
	8. Safu ya (9): andika idadi ya akina baba wanaoishi katika kaya.
	9. Safu ya (10): andika idadi inayoonyesha jinsi ya watu wengine wanaoishi katika kaya.
	10. Safu ya (11): weka alama ya vema (✓) kwenye kisanduku kama mhudumu wa afya ya jamii ngazi ya kijiji ametoa ushauri nasaha kwa mama kuhusu unyonyeshaji maziwa ya mama pekee katika kipindi chote cha miezi 6 ya mwanzo.
	11. Weka alama ya vema (✓) kwenye kisanduku kama mhudumu wa afya ya jamii ngazi ya kijiji ametoa ushauri nasaha kuhusu vyakula vyenye asili ya wanyama na jamii ya kunde (safu ya 12), idadi ya milo na ulaini wa chakula (safu ya 13), Ulishaji shirikishi (safu ya 14), Lishe ya mtoto mgonjwa (safu ya 15). Kama mada tofauti zimejadiliwa weka alama ya vema (✓) katika visanduku vinavyoonyesha mada zote zilizojadiliwa kati ya mhudumu wa afya ya jamii ngazi ya kijiji na mama/mlezi wa mtoto.
	12. Weka alama ya vema (✓) kwenye kisanduku kama mhudumu wa afya ya jamii ngazi ya kijiji ametoa ushauri nasaha kuhusu matumizi ya maji safi toka chanzo salama (safu ya 16), usafi wa mtoto na kumweka mbali na kinyesi cha wanyama (safu ya 17), utupaji salama wa kinyesi cha mtoto (safu ya 18), kunawa mikono kabla ya utayarishaji na ulishaji wa mtoto (safu ya 19) . Kama mada tofauti zimejadiliwa weka alama ya vema (✓) katika visanduku vinavyoonyesha mada zote zilizojadiliwa kati ya mhudumu wa afya ya jamii ngazi ya kijiji na mama/mlezi wa mtoto.
	13. Weka alama ya vema (✓) kwenye kisanduku kama mhudumu wa afya ya jamii ngazi ya kijiji ametoa ushauri nasaha kuhusu mazungumzo na mtoto kwa kutumia ishara na maneno (safu ya 20), kuchezea toys (safu ya 21). kama mada tofauti zimezungumziwa, weka alama ya vema (✓) katika visanduku vinavyoonyesha mada zote zilizojadiliwa kati ya mhudumu wa afya ya jamii ngazi ya kijiji na mama/mlezi wa mtoto.
	14. Weka alama ya vema (✓) kama mhudumu wa afya ya jamii ametoa ushauri nasaha kuhusu matumizi ya vidonge vya kuongeza damu wakati wa ujauzito (safu ya 22), chakula mchanganyiko na cha kutosha (safu ya 23), kumpunguzia kazi ngumu mama mjamzito (safu ya 24). Kama mada tofauti zimezungumziwa, weka alama ya vema (✓) katika visanduku vinavyoonyesha mada zote zilizojadiliwa kati ya mhudumu wa afya ya jamii ngazi ya kijiji na mlezi wa mtoto.
	15. Safu ya (25): andika namba ya simu ya kiganjani ya mkuu wa kaya, au ya mke/mume.
	16. Jumla kuu: katika mstari wa mwisho hapo chini, andika jumla kuu ya idadi toka katika kila safu (safu ya 1-10) au alama ya vema (✓) katika safu hizi (11-24).
JUMLA KUU	Hakikisha taarifa zote zimeandikwa kwa usahihi, kabla ya kuondoka kwenye kaya. Hii itarahisisha zoezi wakati wa kufanya majumuisho na kuingiza taarifa katika mfumo wa kompyuta.

